

Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa
Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

WANATAKA ROHO YAKO

Mfano umetolewa Luka 12:16-21

Mtu mmoja tajiri ambaye alinawiri sana katika fani zote za maisha aliwaza kuhusu siku zake za usoni. Kwa mara nyingine yeye alikuwa amevuna mavuno mengi kutoka shambani mwake, na ndipo akawa na mali nyingi. Alipofikiria kuhusu utajiri huo wake ndipo akafanya mpango kabambe wa kubomoa maghala yake yote ili aweze kujenga maghala mapya makubwa zaidi, na ambayo yangeweza kutoshea kuweka mavuno yake. "Mimi nimefanya kazi sana, na sasa ni wakati wangu wa kufurahia mali hii. Tayari nina pesa za kutosha kunidumisha miaka mingi. Basi nitastaafu nipunge hewa—huku nikila, nikinywa, na kukaa raha mustarehe!" Hayo ndio mawazo ambayo tajiri huyu aliwaza kuhusu siku zake za usoni.

Lakini wakati akitafakari kuhusu kufaulu huko kwake na kuhusu malengo ya siku zizazo, Mungu wa mbinguni, muumba mbingu na nchi, akanena naye akamwambia, "Mpumbavu wewe, usiku huu wa leo wanataka roho yako! Na vitu ulivyojiwekea tayari vitakuwa vyana nani?"

Hata ingawa bwana huyu alikuwa amebarikiwa sana katika maisha haya yetu ya mpito, na pia akawa mwenye mipango kabambe kuhusu siku zake za usoni, yeye aliaga dunia usiku huo huo! Utajiri na kiburi chake havikumsaidia wakati aliposimama na kukondolea macho maisha yake ya milele, wakati ambapo hakuwa tayari kusima mbele ya kitu hicho cha hukumu ya Mungu. Kesho yake haikucha kwa sababu kifo kilipoingia papo hapo yeye alianza safari ambayo haina mwisho, safari ya giza na ya kukata tamaa.

Mungu alimwita mtu huyo mpumbavu kwa sababu alikuwa amepanga mipango mizuri ya maisha haya, lakini alikuwa amepuuza kuiandaa nafsi yake kwa ajili ya maisha

ya milele. Je, mtu huyo anatupatia ujumbe gani kuhusu maisha baada ya kaburi.

"Usimsahau Mungu wako. Maisha ya milele ni ya kweli. Kifo chako hakitakuwa mwisho wako, huo ndio utakuwa ni mwanzo tu." Mbinguni ni mahali ambako kutakuwa na amani na furaha ya ajabu, na mbingu hiyo inawasubiri wale wenye haki; nayo jehanamu, mahali pa mateso na uchungu panawasubiri wenye dhambi. Je, thamani ya mambo ya ulimwengu huu ambao ni wa kupita ni gani wakati ambapo maisha ya milele yanankia? Kifo hakimheshimu mtu ye yote yule. Watu wote, wazee kwa vijana, matajiri kwa maskini, walioelimika na wasioelimika, wanaojulikana na wasiojulikana, watu wote watakuwa na kukutana na Mungu wao. Mambo yanayothaminiwa katika uliwengu huu hayatakuwa na msaada wowote katika maisha yajayo. Jambo muhimu wakati huo itakuwa kama mtu aliachana na dhambi zake. Kama kwamba alimkubali Yesu Kristo kama mwokozi wake? Na kama kwamba alimwishinga Mungu kila siku maishani mwake?

Watu hutumia wakati wao mwangi na nguvu zao nyingi kutafuta utajiri, heshima, elimu, na tamaa za mwili. Pia wao hufanya maamuzi maishani mwao kwa misingi ya manufaa ya maisha ya hapa na sasa, bila kuwaza kuhusu hali ya nafsi zao ambazo ni za milele. Jamii za watu zimemsahau Mungu na wanadamu wanaishi kwa manufaa ya wakati huu.

Hebu basi rafiki yangu ujue kwamba maisha ya milele yako mbele yako, na kwamba maisha hayo hayatakuwa na mwisho, kwa sababu muda na wakati hautakuwa na mpito katika maisha hayo yajayo. Je, wewe uko tayari kukutana na Mungu ambaye atakuhukumu kulingana na jinsi ambavyo umeishi katika maisha haya? Siku hiyo itakapofika wewe autaulizwa

(Endelea katika Ukurasa 2)



"Mambo yanayothaminiwa katika uliwengu huu hayatakuwa na msaada wowote katika maisha yajayo."

MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4,
Efe. 2:1, 5-6

Uhuru Kutokana na Dhambi

1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16,
Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13,
Kol. 1:18

Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,
Yn. 13:14-17

Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,
I Kor. 7:10-11

Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10,
Mt. 25:31-46

Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)

kuhusu familia ulimotoka, hali yako ya kiuchumi, dhehebu lako, au hata mambo ya kidini ambayo uliamini—yote hayo hayatakukomboa kutokana na nguvu za giza la milele. Basi wewe hunu budi kumpokea Yesu Kristo na pia kuishi maisha ya utakatifu (kila siku) mbele zake.



**"Unahitaji kufanya
maamuzi yako ya
kila siku kwa kusudi
la kumpendeza
Mungu na kwa ajili ya
manufaa ya nafsi yako."**

Nabii Amosi aliwaambia wana wa Israeli "(M)jiweke tayari kuonana na Mungu wako" (Amosi 4:12). Huyu kijana tajiri alikuwa amejiandaa kwa ajili ya kustaafu kwake, na jambo hili halikuwa makosa, lakini katika mipango hiyo yake yeeye hakuwa amejiandaa kukutana na Mungu wake. Kujiandaa ni "kujiweka tayari kwa ajili ya ..." Je, wewe umejiandaa kukutana na Mungu? Je, unaishi maisha yako huku ukilia maanani hukumu ya Mungu na maisha yako ya milele? Ili kujiandaa kwa ajili ya jambo fulani inakubidi kufanya bidii. Unahitaji kufanya maamuzi yako ya kila siku kwa kusudi la kumpendeza Mungu na kwa ajili ya manufaa ya nafsi yako.

Ukweli ni kwamba, watu wengi wanapuuza maslahi ya nafsi zao. Wengi wetu tunamjua

Mungu kwa akili tu, huku tukivaa vazi la kidini, lakini maamuzi yetu ya kila siku yanaongozwa na mambo ambayo yatafaidi maisha haya, badala ya kufanya kile ambacho kitafaa kwa maisha yetu ya kiroho. Je, wewe?

Maisha tunayoishi hayana uhakika, na hakuna mmoja wetu ambaye anajua mbeleni siku yake ya kufa na kukutana na Mungu. Hebu basi tusiwe wa kuishi maisha kama ya mtu huyo mpumbavu. "Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yake? Au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake?" (Mathayo 16:26). Wakati tutakapokufa na kusimama mbele ya kiti cha hukumu ya Mungu, huku tukiwa tumepuuza swala la kumweka Mungu nambari moja maishani mwetu, ni kitu gani ambacho tutakuwa tayari kulipia ili tupate maisha ya milele? Ukweli ni kwamba, wakati huo tutakuwa tayari kutoa chochote kile, hata mali yetu yote, ili kuepuka uchungu wa jehanamu. Katika maisha hayo ya milele kila mtu atakuwa yu radhi kuishi maisha mara nydinge kama angalipewa nafasi ya kufanya hivyo. Watu watakuwa tayari kubadili mienendo yao na kutoa kila chote walicho nacho na ambacho kiliwazuia kuishi maisha matakatifu na ya kitauba maishani haya. Kwa kweli watakuwa tayari kusalimisha maisha yao yote, elimu zao, anasa zao, na hata mielekeo yao yote ambayo iliwayeka akili na kuwatenganisha na Mungu. Lakini kamwe hawatapata nafasi ya pili ya kujiandaa kwa ajili ya maisha ya milele. Sasa ndio wakati wetu; hii ndio nafasi yetu.

Na wewe je? Utafanya nini na nafsi yako sasa? Kama unaishi maisha yako kwa ajili ya manufaa ya mambo ya ulimwengu huu badala ya kuishi kila siku huku ukimtumikia Mungu, na kwa kuwahudumia wanadamu wenzako tumaini kuu la Mungu, kuna haja kubwa ya kunyenyekoa moyoni mwako na kumwomba Mungu. Hebu basi mpokee Yesu moyoni mwako na ufanye maamuzi maishani mwake kwa njia ambayo haiongozwi na manufaa ya maisha ya ulimwengu huu wa mpito; na badala yake uwe wa kuongozwa na ulimwengu wa milele ambaa unakuja kwa haraka. Wakati uliobaki ni mdogo sana, na Bwana Yesu Kristo anakusubiri. ■

Gazeti la Ukweli wa Injili ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tudembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uwee kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la Ukweli wa Injili linachapishwa katika nchi nydingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kuititia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako. —Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@gospeltruth.org

Tahariri



Akatoka nje akalia kwa majonzi. —Luka 22:62

Wakati Yesu alipokuwa akifanyiwa mashtaka, Petro (ambayo alikuwa amemfuata kwa umbali mrefu) aliweza kumkana mara tatu. Hapo baadaye Petro alitoka nje ya ukumbi na kulia machozi mengi. Yeye alivunjika moyo na kuhuzunika sana kwa sabau ya kumkana Bwana na Mwokozi wake. Lakini urembo wa hadithi hii ni kwamba tukio hilo halikuwa mwisho wa hadithi ya Petro. Wakati Yesu alipofufuka, Yeye alitaka hasa Petro kujua kwamba sasa Yeye yu hai. Hata ingawa Petro alikuwa amemkana Bwana, Mungu alikuwa amekubali roho yake ya toba, na ndiposa Petro akaweza kupata nafasi nyingine ya kumtumikia Yesu. Mungu wetu apewe utukufu wote!

Somo la robo hii ya mwaka linahusu swala la toba, toba ambayo inafundishwa katika biblia. Hata ingawa kuna toba ambayo inafanyiwa kitaifa, kifamilia, na hata kikanisa—tleo hili haswa linashughulika na mafundisho ya Biblia kuhusu kutubu kwa mtu kibinagsi. Shauku la moyo wangu ni kwamba, laiti kungalikuwa na huzuni kubwa kwa ajili ya dhambi ambazo watu wanafanya. Watu huingia taabani maishani mwao na kugeuka na kuingia katika mambo ya kidunia huku wakitafuta suluhisho maishani mwao, lakini kamwe hawapati suluhu hiyo. Jawabu linalofaa ni watu kupiga magoti na kwa huzuni kubwa miyoni mwao wamtafute Mungu ili aweze kuwapa msamaha.

Wakati kutakopatikana toba ya kibinagsi ndipo ndoa zetu zitarudishiwa hali bora ya afya yake, mahusiano ya watu yatafanyiwa upya, makosa ya mtu mmoja kwa mwingine yatasamehewa, na utakatifu utajaa kote. Ukosefu wa mambo hayo katika jamii zetu unatokana na ukweli kwamba watu hawaonei dhambi zao huzuni, na pia hawafanyi toba. Mara nyingi makundi ya kidini hufundisha kuhusu Kristo, lakini yanakosa kusema lolote kuhusu haja ya watu kutubu. Ni ombi langu kwamba wahudumu wa kweli wa Injili ya Mungu hawatakoma kuhubiri kuhusu haja ya watu kutubu. Wengi wetu tunataka kupata baraka za Mungu, lakini mara nyingi hatutaki kulipa gharama ya kupata baraka hizo. Kuna ujuzi wa Kikristo amba ni zaidi ya mtu kuomba (siku baada ya nyingine) kupata msamaha wa dhambi zake. Je, tutahubiri watu watoke dhambini lakini muda si muda wao warudi katika mambo ya kidunia? Hapana! Wewe Mkristo, achana na dhambi zako! Kuna nguvu katika damu ya Kristo ya kukwezesha kuishi maisha ya ushindi dhidi ya nguvu na adhari za dhambi katika dunia hii.

Mimi hubarikiwa sana kuona watu wakiomba na kupokea wokovu, na pia hufurahi kusikia watu kama hao wameanza kumuishia Mungu. Lakini wakati mwingi mimi huona kwamba ujuzi wa wengi wa watu hao hauwi wa kudumu. Ni imani yangu kwamba jambo hili kusababishwa na watu kukosa kutubu. Tunahitaji kuelewa upotovu wa kupita kiasi amba unaletwa na dhambi na watu kutomtii Mungu, na kwa hivyo tuweze kuachana na mambo hayo yote huku tukiwa na huzuni kubwa miyoni mwetu. Kwa furaha kuu miyoni mwetu tunahitaji kumkumbatia Mwokozi wetu. Ikiwa tunataka kupata ujuzi wa kudumu wa wokovu wetu hatuna budi kuachana na dhambi kabisa kabisa.

Ikiwa wewe unaendelea kutenda dhambi basi bado haujaokoka. Haijalishi jinsi watu wengine wanavyowaza kuhususiana na maisha yako ya kiroho, wewe mwenyewe wajijua kama kwa kweli u mwenye dhambi; kama umerudi nyuma; au kama u mnafiki; au kama kweli wewe ni mtakatifu wa Mungu. Kama katika dhamiri na moyo wako unajihisi hatia mbele zake Mungu basi ninakuomba uchukue mweke huu kutubu. Achana na dhambi ambayo inakwandama na umpatie Bwana asilimia mia moja (100%) ya moyo na maisha yako. Yeye ni mwaminifu na atakusaidia kudumisha wokovu wako na utakua katika mambo ya Kikristo. Je, wewe utatubu leo bila kuchelewesha jambo hilo? Je, utamwomba Mungu?

Michael W. Smith

Oktoba 2021.

IKIWA WATU WANGU, WALIOITWA KWA JINA LANGU,
WATAJINYENYEKESHA, NA KUOMBA, NA KUNITAFUTA USO,
NA KUZIACHA NJIA ZAO MBAYA; BASI, NITASIKIA TOKA MBINGUNI,
NA KUWASAMEHE DHAMBI YAO, NA KUIPONYA NCHI YAO.

– 2 MAMBO YA NYAKATI 7:14



Mwongozo wa Kujifunza Biblia

Somo: KUTUBU

Somo la Maandiko: *Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe.* —Matendo 3:19

Maana:

Kutubu: Kubadilisha kauli; kufanya marekebisho kwa moyo wako wote, huku ukichukia moyoni mwako dhambi zako za hapo awali (Kamusi ya Maandishi ya Kiyunani ya Thayer).

Toba: Kuvunjika moyo au kujuta kwa ajili ya matendo maovu ambayo mtu alifanya hapo mbeleni, kubadilisha kauli, kuachana au kutoka dhambini na kukumbatia mambo ambayo yanampendeza Mungu.

Muhstasari: Mungu anawaita wenye dhambi wote kutubu na kuachana na dhambi zao. Ujumbe wa Injili ni kwamba sote tunahitaji kukataa na pia kuachana uovu wote na kumfuata Yesu katika utakatifu wote. Kama mtu hajatubu basi ye ye angali bado hajapata wokovu wa kweli.

I. Ni Nani Ambaye Anahitaji Kutubu

- A. Mathayo 9:12-13 Wenye dhambi.
- B. Matendo 17:30 Watu wote wa kila mhali.

II. Mahubiri Kuhusu Toba

- A. Luka 3:3 Yohana Mbatizaji-toba ya ondoleo la dhambi.
- B. Marko 1:14-15 Yesu—tubuni na kuamini injili.
- C. Marko 6:12 Wanafunzi wa Yesu waomba watu kutubu.
- D. Matendo 20:20-21 Paulo—kutubu kwa Mungu.

III. Haja ya Mtu Kutubu

- A. Luka 13:3 Majina yameandikwa Mbinguni.
- B. Matendo 3:19 Ili dhambi zenu zifutwe.
- C. Ufunuo 2:5 Ili mpate baraka za Mungu na upako wake.

IV. Tunda la Toba

- A. Luka 3:8 Toeni matunda yapatanayo na toba.
- B. Matendo 26:19-20 Kutenda matendo yanayopatana na toba.
- C. Yakobo 4:8 Itakaseni mikono yenu enyi wenye dhambi.

V. Sifa Nambari Moja ya Toba: Huzuni

- A. 2 Wakorintho 7:9-11 Huzuni ya Kiungu humfanya mtu kutubu.
- B. Zaburi 51:17 Moyo uliovunjika na kupondeka.

VI. Sifa Nambari Mbili ya Toba: Kuungama Dhambi

- A. 1 Yohana 1:9 Tukiziungama dhambi zetu.
- B. Mithali 28:13 Yeyote aziungamaye na kuziacha.

VII. Sifa Nambari Tatu ya Toba: Kuachana na Dhambi

- A. Isaya 55:6-7 Mtu mbaya aachane na njia zake.
- B. Ezekieli 18:30 Achaneni na makosa yenu yote.

VIII. Sifa Nambari Nne ya Toba: Kuachana na Uovu

- A. 2 Wakorintho 6:14-18 Mkatengwe nao.
- B. Ezekieli 14:6 Mkageuke na kuviacha vinyago vyenu.

IX. Sifa Nambari Tano ya Toba: Kurudisha

- A. Walawi 6:4-5 Kurudisha ulichochukua.
- B. Luka 19:8-9 Zakayo alirudisha alichochukua.

X. Mifano ya Toba

- A. Luka 15:21 Mwana Mpotevu—“nimekosa juu ya mbingu.”
- B. Luka 18:13 Mtoza Ushuru—“Ee Mungu, uniwie radhi mimi mwenye dhambi.”
- C. Yona 3:8 Ninewe—“Kila mtu akaacha njia yake mbaya.”

XI. Wito wa Toba

- A. Matendo 2:37-40 Tubuni . . . Jiokoeni.
- B. Ufunuo 3:19 Basi uwe na bidii, ukatubu.

XII. Nafasi ya Kufanya Toba

- A. Ufunuo 2:21 Mungu alitoa muda wa kutubu.
- B. 2 Wakorintho 6:2 Siku ya wokovu ndio sasa.
- C. Warumi 2:4 Wema wake Mungu.
- D. 2 Petro 3:9 Mungu hapendi mtu ye yote apatee.

Tamati

Nawaambia, vivyo hivyo kutakuwa na furaha mbinguni kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye, kuliko kwa ajili ya wenye haki tisini na kenda ambaao hawana haja ya kutubu.

—Luka 15:7

TOBA

AMBAYO INAFUNDISHWA KATIKA BIBLIA

Achana na dhambi, kataa maovu, okolewa na nguvu za Mungu. Mahali kote ambako ujumbe wa Yesu Kristo unahubiriwa ujumbe wa toba hauna budi kuhubiriwa; hii ni kwa sababu bila toba hamna wokovu wa kweli.

Kugeuka Kabisa

Kutubu ni jambo ambalo linafanyika wakati mtu amehuzunishwa na dhambi zake za hapo awali, jambo ambalo humfanya aache dhambi hizo na kuanza kumfuata Kristo. Toba ya kweli humbidi mtu kufanya uamuza wa kuacha makosa yake, na pia kufanya uamuza

kwamba hatorudi katika maisha hayo ya dhambi.

Maana kamili ya kutubu ni mtu kuacha njia za hapo awali na kubadilisha mwenendo wake. Lakini makanisa mengi ya Kikristo humhubiri Yesu Kristo akiwa toleo la dhambi bila wao kuhubiri ujumbe wa toba. Ni jambo moja mtu kumpokea Kristo, lakini ni jambo tofauti kabisa mtu kubadili mwenendo wake na kuacha mambo ambayo hayampendezi Mungu. Hata ingawa mtu hapati wokovu kuititia kwa matendo yake mema, kwani wokovu ni kipawa cha kiungu

cha Mungu, lakini tunalo jukumu la kutekeleza. Mtume Petro aliwaambia wasikilizaji wake, "Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana" (Matendo 3:19). Mungu atawasamehe wale ambao wanachukulia wokovu wao kwa makini hivi kwamba wako tayari kuachana na mambo yote ambayo sio ya kiungu.

Yesu alikuja ulimwenguni na kufa kwa ajili ya wanadamu wote ili watu wapate kuokolewa "Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu" (Warumi 3:23). Yeye alikuja kuwaita "wenye dhambi" kutubu (Mathayo 9:13), na Mungu "anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu" (Matendo 17:30). Hakuna mtu ye yote ambaye hajaamriwa kutubu, kwa maana watu wote wametengwa na Mungu kutokana na dhambi zao na pia makosa yao. Bila kuchukia makosa tunayofanya dhidi yake Mungu, bila

kuhuzunika kwa ajili ya mambo tuliyotenda na ambayo yalitutenganisha na Mungu, mtu hawezo kupata wokovu.

Ni Sehemu Muhimu ya Ujumbe wa Wokovu

Ujumbe wa kutubu haukuwa ujumbe wa kuhubiriwa mara moja tu mahali fulani pembeni. Yohana Mbatizaji, ambaye ndiye alikuwa mtangulizi wa Kristo: "Akafika nchi yote iliyo karibu na Yordani, akihubiri ubatizo wa toba liletalao ondoleo la dhambi" (Luka 3:3). Yesu naye alihubiri Injili ya Ufalme wa Mungu kwa ujumbe dhabiti: "Tubuni, na kuiamini Injili" (Marko 1:14-15). Wanafunzi wa Yesu nao walitumwa "Wakatoka, wakahubiri kwamba watu watubu" (Marko 6:12). Mtume Paulo anasema kwamba "Nikiwashuhudia Wayahudi na Wayunani wamtubie Mungu, na kumwamini Bwana wetu Yesu Kristo" (Matendo 20:21). Basi ujumbe huu wa toba ni tofauti na ujumbe ule rahisi wa kumwamini Yesu, ambao humwondolea mwanadamu jukumu la kufanya mabadiliko maishani mwake. Ndiposa makanisa mengi ya uongo katika siku zetu huhubiri kwamba mtu hawezo kuishi bila kutenda dhambi. Lakini nguvu za ujumbe wa Injili ni kwamba, kuititia kwa kutubu na kumwamini Kristo mtu upata nguvu hivi kwamba maisha yake yanakuwa ya kutii agizo la "usitende dhambi tena" (Yohana 8:11).

Inahitajika Ili Mtu Apate Wokovu

Kutubu ni sehemu muhimu ya ujuzi wa kupokea wokovu ili mtu aweze kupata uzima wa milele. Katika Luka 13:3 Yesu alisema kwamba "Msipotubu, ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo." Haitoshi tu mtu kuijunga na ushirika fulani wa kidini na kumwabudu Mungu kwa kuvaa vazi la mfano wa utauwa. Ni lazima mtu apate ujuzi ambao unabadilisha maisha yake kabisa, ujuzi ambao huanza kwa mtu kutubu kibinagsi. Hii ndio njia ya pekee ya kufanya watu: "dhambi (zao) zenu zifutwe" (Matendo 3:19). Watu wasipotubu upako na baraka zake Mungu zitaondolewa kutoka katikati mwao na kutoka kwa makanisa yao ambayo tayari yasharudi nyuma na kuanguka. Mfano bora wa jambo hili katika Biblia unapatikana katika kanisa la Efeso ambalo linaambiwa: "Basi, kumbuka ni wapi ulikoanguka; ukatubu, ukayafanye matendo ya kwanza. Lakini, usipofanya hivyo, naja kwako, nami nitakiondoa kinara chako katika mahali pake, usipotubu" (Ufunuo 2:5).

Yohana Mbatizaji naye alionya Mafarisayo "Basi, toeni

(Endelea katika Ukurasa 6)

Toleo 31 | www.thegospeltruth.org

matunda yapatanayo na toba; wala msianze kusema miyoni mwenu, tunaye baba, ndiye Ibrahim” (Luka 3:8). Cheo cha mtu na kutambulika kwake hakuwezi kumweka huru na kumwondolea haja ya kutubu. Kuna watu ambao wamo katika uongozi wa vikundi nya kidini ambao wanahitaji kunyenyeka katika miyo yao na kumlilia



Mungu. Wachungaji, waimbaji, na waalimu wataangamia na kupoteza nafsi zao ikiwa hawataacha dhambi zao za hadharani na za maisha yao ya kibinafsi kwa miyo ulyovunjika.

“Basi kutubu ni jambo ambalo linambidi mtu kuachana na miungu ya uongo ya kisasa kama vile utajiri, mavazi ya kisasa, michezo, mambo ya burudani, n.k. yote ambayo huteka miyo na akili za watu wa dunia.”

Ni jukumu letu kuzaa matunda yanayotokana na toba yetu—huku miyo na nia zetu zikibadilika na kufuatwa na maneno (pamoja) na matendo yetu. “Watubu na kumwelekea Mungu, wakiyatenda matendo yanayopatana na kutubu kwao” (Matendo 26:20). “Itakaseni mikono yenu, enyi wenye dhambi” (Yakobo 4:8), na kumgeukia Bwana ili muweze kupata wokovu.

Huzuni ya Kiungu

Kutubu ni neno ambalo lina maana nyingi na ambalo huwa na sifa na tabia aina aina. Lakini mtu kuwa na huzuni ya kiungu moyoni mwake ni sehemu muhimu ya kutubu na ndilo jambo ambalo humletea mtu wokovu. “Maana huzuni ilio kwa jinsi ya Mungu hufanya toba lilelalo wokovu lisilo na majuto; bali huzuni ya dunia hufanya mauti. Maana, angalieni, kuhuzunishwa kuko huko kwa jinsi ya Mungu kilitenda bidii kama nini ndani yenu; naam, na kujiteeta, naam, na kukasirika, naam, na hofu, naam, na shauku, naam, na kujitahidi, naam, na kisasi! Kwa kila njia mmejionyesha wenyewe kuwa safi katika jambo hilo” (2 Wakorintho 7:10-11). Kwa kweli huzuni ilio ya jinsi ya Mungu ni zaidi ya huzuni ya kilimwengu ambayo mtu hujihisi kuhukumiwa kwa sababu ya kufanya makosa lakini anaendelea na njia zake za kufanya makosa. Huzuni ya kiungu inambidi mtu kuvunjika moyo, na inafanya mtu huyo kubadilika. Mungu naye hukubali na kuipokea huzuni hiyo na kunyenyeka kwa mtu huyo, “Dhabihu za Mungu ni roho iliyovunjika; moyo uliovunjika na kupondeka” (Zaburi 51:17).

Kukiri na Kuacha

Kutubu ni jambo ambalo linahusisha mtu kukiri na kutambua dhambi ambayo ametenda kwa njia ya uwazi. Bila kukiri hamna msamaha. Yohana wa Kwanza 1:9 inasema “Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.” Lakini “Afichaye dhambi zake hatafanikiwa; bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema” (Mithali 28:13).

Mtu kukiri dhambi zake bila kuacha dhambi hizo ni jambo ambalo halina maana; jambo lisilo na faida hata kidogo. Kuna watu wengi ambao hukiri dhambi zao lakini huwa hawako tayari kuziacha. Lakini Maandiko yako dhahiri kuhusiana na swala hili, “Mtu mbaya na

aache njia yake, na mtu asiyehaki aache mawazo yake; na amrudie BWANA, naye atamrehemu; na arejee kwa Mungu wetu, naye atamsamehe kabisa” (Isaya 55:7). Hata katika Agano la Kale nabii Ezekiel aliwaambia wasikilizaji wake “Basi, nitawahukumu ninyi, nyumba ya Israeli, kila mmoja kwa kadiri ya njia zake, asema Bwana MUNGU. Rudini, mkaghairi, na kuyaacha makosa yenu yote; basi hivyo uovu wenu hautakuwa uharibifu wenu” (Ezekiel 18:30). Kwa kweli dhambi zako zitakuangamiza ikiwa hutaachana nazo.

Ishara nyingine ya mtu kuacha dhambi kwa sababu ya toba ya moyoni ni kwa mtu kama huyo kujitenga na uovu wote na madhara yanayoletwa na uovu huo ulimwenguni. Mtume Paulo alitoa mwongozo kwa kanisa la Korintho ili wajitenge na mahusiano na watu wasioamini, ibada ya sanamu, na uchafu wote (2 Wakorintho 6:14-18). Naye nabii Ezekiel aliwaagiza watu wa Israeli “Rudini ninyi, mkageuke na kuviacha vinyago vyenu” (Ezekiel 14:6). Basi kutubu ni jambo ambalo linambidi mtu kuachana na miungu ya uongo ya kisasa kama vile utajiri, mavazi ya kisasa, michezo, mambo ya burudani, n.k. yote ambayo huteka miyo na akili za watu wa dunia.

Fanya Mambo Kuwa Sawa

Kulipa fidia au kurudisha kitu ulichochukua hapo awali ni sifa nyingine au tunda la kutubu. Zakayo alipoahidi atawarudishia watu pesa ambazo alikuwa amewanyang’anya Yesu alimjibu na kusema “Leo wokovu umefika nyumbani humu” (Luka 19:8-9). Kurudisha ni tendo la kurekebisha makosa ya hapo awali na ni ishara ya toba ya kweli ambayo huwa ni motisha ya matendo ya mtu kama huyo.

Maandiko yanaonyesha urembo wa toba ya kweli. Mwana Mpotevu alifungua kinywa na kusema “Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena” (Luka 15:21). Mtoza ushuru ambaye alikuwa akiomba katika hekalu alihesabiwa haki kwa sababu (hata) hangeweza kufungua macho yake kuelekea mbinguni na badala yake akamlilia Mungu akisema “Uniwie radhi mimi mwenye dhambi” (Luka 18:13). Nazo rehema za Mungu zilifika katika mji wa Nineve wakati ambapo mji huo ulitubu na kuachana na njia za uovu (Yona 3:8). Mungu ni mwenye rehema na Yeye anawapatia wenyewe dhambi nafasi ya kutubu (Ufunuo 2:21) na anawapokea kwa furaha na sherehe huko mbinguni kwake wanapofanya hiyvo (Luka 15:7). Yeye “huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apatee, bali wote wafikilie toba” (2 Petro 3:9).

Basi Tubu Leo

Siku moja uvumilivu huo wa Mungu utafika mwisho, na siku ya hukumu itaingia. Ujumbe ambao Petro alihubiri katika siku ya Pentekote ungali ndio ujumbe tunastahili kukiapatia kizazi hiki chetu: “Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu” (Matendo 2:38). Basi kama wewe ungali bado hujatubu Mungu anakwambia, “Siku ya wokovu nalikusaidia; tazama, wakati uliokubalika ndio sasa; tazama, siku ya wokovu ndiyo sasa” (2 Wakorintho 6:2). Kuna amani na pumziko ambalo mtu hupata tu kwa njia ya toba ya kweli. ■

“Sio kazi ya Mungu ambayo si kamili, bali ni ukosefu wa toba kabla ya mtu kupokea wokovu.”

Ni Nini Umuhimu wa Toba Katika Wokovu?

Kulingana na Maandiko kutubu ni jambo ambalo limefunganishwa kabisa na ujuzi wote wa wokovu. Yesu aliwaambia wasikilizaji wake “tubuni . . . na kuiamini injili” (Marko 1:15). Bwana Mungu alitoa mweke wa sisi kuweza kupata wokovu kuititia kwa kifo cha Yesu msalabani. Yeye yuko tayari kutusamehe dhambi zetu na kutupatia kipawa cha uzima wa milele. Lakini kipawa hicho hutolewa kwa watu wale ambaeo wanaonea majonzi makosa yao na ambaeo “Lakini ikiwa mtu atatafuta wokovu bila toba ya kweli

wanafanya uamuzi wa kibinafsi wa kuachana na dhambi hizo.

yeye hatakuwa imara katika wokovu wake. Wale ambaeo watamwomba Mungu wokovu lakini hawana toba ya kiungu

hawataweza kupata ujuzi unaobadilisha maisha yao. Ni lazima kuwe na shauku la kuachana na dhambi na kumfuata Kristo. Yesu alimwambia kijana mmoja tajiri ambaye alitaka kumfuata kwamba aende kwanza auze mali yake. Kama kijana huyo angemtii Yesu hii ingekuwa ishara ya tunda la toba na pia ishara ya kwamba yeye alikuwa tayari kuacha yote kwa ajili ya Kristo. Lakini kijana mwenyewe hakuwa tayari kuachana na mambo ya kidunia.

Wakati mwingi watu hukiri kumwamini Yesu Kristo lakini wanaendelea katika dhambi zao. Kwa kweli watu kama hao hawajaokoka, kwa sababu wokovu hutolewa tu kwa wale wenye miyo ya toba. Huenda ikawa kuna shauku ya mwanzo mwanzo ya mtu kutaka kubadilika, lakini ikiwa mtu atatafuta wokovu bila toba ya kweli yeye hatakuwa imara katika wokovu wake. Ni lazima mtu atambue makosa yake na pia ahuzunike kwa ajili ya kukosa kumpendeza Mungu. Pia ni lazima mtu awe na shauku ya kuachana na dhambi za hapo awali; na kama mtu hana shauku kama hiyo basi dhambi hizo zitarudi maishani mwake. Jambo hilo likitendaka watu hufikiria kwamba ni kazi ya wokovu wa Mungu ambayo haikuwa kamili. Lakini ukweli ni kwamba, sio kazi ya Mungu ambayo si kamili, bali ni ukosefu wa toba kabla ya mtu kupokea wokovu. Basi toba ni jambo muhimu sana katika wokovu, kwa maana bila toba mtu hawezi kukombolewa kutoptana na nguvu za dhambi.

Mwenye dhambi anahitaji kwanza kufungua moyo wake kwa Mungu na kukataa maovu yote. Jambo hili ndilo hufungua mlango ili Mungu aweze kufanya muujiza wa kumletea mtu huyo wokovu ambaeo utamwezesha kwenenda katika maisha mapya. Hii ndiyo sababu Yesu aliwaomba halaiki ya watu ambaeo walikuwa wamemzunguka kwamba wahesabu gharama ya kumfuata. Hebu nawe tafakari maana ya kuchukua msalaba wako na kumfuata Yesu. Waza kuhusu jambo hilo kwa makini kabisa kabla ya kufanya uamuzi wa kupokea wokovu. Utakapoamua kwamba uko tayari kumpatia Mungu mambo yote kwa njia ya kutubu, hapo ndipo utakafungua mlango wa kupata neema yote ya wokovu wa Mungu.

Je, Mimi Nikijihisi Vibaya kwa Sababu ya Dhambi Zangu - Hii Ni Kuonyesha Kwamba Nimetubu?

La, hasha. Mtu ambaye hana moyo wa toba anaweza kujihisi vibaya au kuhuzunika kwa sababu ya kutenda dhambi, lakini jambo hilo halitamletea mabadiliko yanayoletwa na toba. Hebu fikiria kuhusu mtu ambaye anamdhulumu mkewe na ambaye baada ya kufanya matendo hayo ya dhuluma analia machozi mbele ya mkewe na kumwambia kwamba amehuzunika sana kwa sababu ya kumdhulumu kwa njia hiyo, jambo ambalo chanzo chake kilikuwa ni hasira za ulevi. Lakini huzuni kama hiyo hudumu wakati tu mtu huyo bado hajalewa tena, akilewa mara nyingine yeye hurudia tabia hizo za dhuluma. Hii ni aina ya huzuni ya kilimwengu. Lakini huzuni kwa Mungu (2 Wakorintho 7:10) ndiyo ambayo humpa mwenye dhambi shauku kubwa ya kubadilisha mienendo yake, bila hata kuhesabu gharama ambayo inambidi kulipa. Wakati ambapo mtu amehakishiwa jambo na Roho Mtakatifu, yeye anaweza kujihisi vibaya na hata kulia kwa kutambua kwamba anaishi katika dhambi. Lakini machozi au hisia za kujuta sio tosha. Ni lazima kuwe na huzuni ya kiungu ya mtu kutambua makosa yake, jambo linaloandamana na nia ya mtu ya kutorudi katika maisha ya dhambi. Huzuni ya aina hiyo ndiyo ambayo humletea mtu toba ya kweli.



JE, WAJUA?

Wakati nabii Yona alihubiri katika mji wa Ninewe na kusema kwamba mji huo ungeangamizwa baada ya siku arobanne, watu hao walimwamini Mungu na kujitangazia siku za mfungo. Hakukuwa kiumbe katika mjo huo, iwe mwanadamu au mnyama, ambacho kilikula chakula au kunywa maji. Wote walivaa magunia kama ishara ya kuvunjika moyo na kutubu! Mungu naye akaokoa mji huo! (Yona 3:4-10).



WEMA WA MUNGU

Au waudharau wingi wa wema wake na ustahimili wake na uvumilivu wake, usijue ya kuwa wema wa Mungu wakuvuta upate kutubu? —Warumi 2:4

Hakuna njia a ambayo mwanadamu anaweza kuepuka hukumu ya Mungu, kwani "Sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu" (Warumi 14:10). Lakini kwa rehema zake Mungu, ambazo hazina mwisho, Bwana anachelewesha siku hiyo ili watu wengi zaidi wawewe kuokolewa kutokana na nguvu za dhambi na kupata mweke wa kuijandaa kwa ajili ya maisha yao ya milele. Rehema za Mungu zimefunguliwa na kumfikia hata mtu yule mwovu kabisa, na upendo wake unawafikia hata wale amba wamedharauriwa sana katika jamii. Yeye huwarehemu wenye dhambi amba wanachukiza zaidi, na anawajali hata watu wale amba wamelaaniwa na kukataliwa na jamii zao.



Lakini watu wengi hudhifikasi wema huo wa Mungu kwa njia ya kudharau upendo na uvumilivu wake na wanakataa kukubali mpango wa wokovu amba ni wa kupendeza sana. Kwa kweli wema wa Mungu ndio hufanya watu kukubali na kutubu dhambi zao. Wakati macho ya mtu yamefunguliwa na anaweza kuona upendo wa Mungu na karama yake ya uzima wa milele, moyo wake hufanywa mwepesi, jambo linalozua shauku ndani yake ya kukumbatia vipawa vyote vya Mungu.

Kusema kweli sisi hatustahili wema wa Mungu, subira zake, na huruma zake, kwa sababu sisi sote tumekuwa katika hali ya kumuasi Mungu. Lakini ni katika hali hiyo ya kumkataa Mungu ndipo Yeye mara nyingi hudhihirisha jinsi ambavyo anatuji. Wakati ambapo matendo ya watu yanastahili hukumu kwa sababu ya madhara na uchungu amba wao wanawaletea wenzao, ni wakati huo ambapo Mungu huwaonyesha huruma na subira zake. Yeye anachelewesha hukumu zake na kukatisha adhabu yake kutokana na wema wake amba hauna kifani. Utajiri wa wema wake nao hudhihirika muda baada ya mwingine, kwa sisi wanadamu amba tumeanguka.

Je, ni kwa nini Mungu huwa mvumilivu kiwango hiki? Ni kwa nini Yeye huwa mwema sana kwa watu wakati ambapo wao hawastahili? Hii ni kwa sababu wema huo na upendo wake ndio mambo ambayo huvuta wanadamu na kuwashimiza kubadilisha mienendo yao. Sifa hizo za Mungu wetu ndizo hufanya watu kuacha makosa yao na kufuatilia mambo yale ambayo yanampendeza Bwana wetu.

Mlango wa rehema u wazi, na msamaha unawasubiri mtu yeoyote yule ambaye ana moyo wa toba. Hebu basi tumsifu Mungu kwa wema wake! ■